

TUMEUMBWA KUMWABUDU MUNGU

ISAYA 43:7

- Ikumbukwe kwamba wanadamu tumeumbwa ili tumwabudu Mungu – Tumpe Mungu Utukufu
- Na, ikiwa Mungu hajaabudiwa, wanadamu wataabudu kitu kingine kama vile pesa, cheo, mtu viumbe vingine, miungu...
- Hata hivyo, mioyo yao haitatoshelezwa hadi pale watakapomwabudu Mungu wa kweli – Muumbaji

Tumeubwa Kumwabudud Mungu...

- Ili kumwabudu Mungu kwa ubora zaidi, inahitaji kufanya hivyo katika **UJUMLA WOTE WA MTU - WARUMI 12:1-2:** (mwili, akili, nguvu, muda, ujuzi...)
- Kumwabudu Mungu katika ubora kunatubadilisha na kutupa mahusiano zaidi ya karibu na Mungu – **MATHAYO 18:19-20**
- Ndio maana Biblia inatuhimiza kumwabudu Mungu huku tukimpa sifa na utukufu peke yake
- Kumwabudu Mungu kunaweza kufanywa na mtu binafsi au katika kundi la pamoja la waaminio.

Njia Tofauti Zinazotumika Kumwabudu Mungu

- **Kumwabudu Mungu Kupitia Muziki** – muziki, nyimbo, na kucheza kwa ajili ya Bwana - iwe ni sehemu ya kuonyesha sifa na shukurani zetu kwa Mungu
- **Kumwabudu Mungu Kupitia Maombi** – maombi yetu siku zote yampe Mungu sifa na shukurani kwa kumaanisha
- **Kumwabudu Mungu Kupitia Roho Mtakatifu** – njia hii inatusaidia wakristo kupokea pumziko na utoshelevu wa kiroho
- **Kumwabudu Mungu Kupitia Utoaji** – **niombe tuchukue muda kidogo kujifunza kwenye hii njia.**

Kumwabudu Mungu Kupitia Utoaji

- Utoaji kwa Mungu ujulikane kuwa ni sehemu ya ibada na kuabudu kwetu mbele zake
- Ni tendo la shukurani, utii na heshima kwa Mungu – **MITHALI 3: 9-10**
- Utoaji kwa Mungu ufanyike kwa moyo wa Upendo, Utayari, Shukurani, na Uwezo –**KUTOKA 35: 20-29**
- Utoaji kwa Mungu ufanyike huku tukijua kuwa vitu vyote ni mali ya Bwana – **ZABURI 24:1**
- Hivyo basi, tutiwe moyo kuzidi kumwabudu Mungu siku zote na hasa kupitia njia ya UTOAJI.